# KUPAKWA MAFUTA NA ROHO OVU YA UONGO

*Maana ile siku ya kuasi hivi sasa inatenda kazi, lakini yuko azuiaye sasa, hata atakapoondolewa hapo ndipo atakapofunuliwa yule asi, ambaye Bwana Yesu atamwuua kwa pumzi ya kinywa chake na kumwangamiza kwa ufunuo wa kuwepo kwake; yule ambaye kuja kwake ni kwa mfano wa kutenda kwake shetani, kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli wapate kuokolewa. Kwa hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu wauamini uongo; ili wahukumiwe wote ambao hawakuiamini kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu (2Wathesalonike 2:7-12).*

Hebu tusikilize kile nabii wa Mungu alichosema; aliulizwa; *siwezi kujisalimisha kikamilifu kwa yesu. Je ninayo roho ovu?*

Hebu nichukue muda wote uliobakia katika hilo pale. Huwezi kujisalimisha kwa yesu? Unaona, sijui mwanaume au mwanamke;siwezi kuelewa ni nani. Mungu anajua hilo.

Huwezi kujisalimisha kwa Yesu kwa nini? Kuna shida gani? Kama wewe ni mwanamke, wewe hujisalimishi kwa mumeo ili kuwa mkewe kwa kujisalimisha vyote ulivyo? Msichana mdogo ulipoolewa, msafi/bikira, ulipigana maisha yako ubakie msafi/bikira, lakini siku moja ulimpata mwanaume mmoja ambaye ulimpenda. Ulikuwa wake kabisa. Vitu vyote ulivyovipigania, kushindania katika maisha yako na kujaribu kuishi msafi na bila lawama na Bikira, sasa unavisalimisha kabisa katika mikono ya mwanaume huyu mmoja. Je hiyo ni sawa? Unajiweka kikamilifu mikononi mwake; u wake. Vile vyote ulivyosimamia kuwa na mazoea mazuri na mwenendo na uadilifu na kila kitu kama hivyo, sasa unavigeuzia kwa mwanaume mmoja kwa sababu unajisalimisha mwenyewe kwa mwanaume. Je huwezi kufanya jambo hilo hilo kwa Yesu kristo? Jisalimishe tu mwenyewe hivyo, “Vile vyote nilivyo, akili yangu yote, mawazo yangu yote” hakika.

Sifikirii kwamba umeshikwa na roho ovu; nafikiri kwamba roho ovu inakupaka upako na mawazo ya aina hiyo ikikufanya ufikiri kwamba huwezi kujisalimisha mwenyewe kwa Mungu. Ngoja nikuonyeshe jambo fulani kwa nini unapenda kusalimisha maisha yako kwake? Kwa sababu kuna kitu pale kinachokuita wewe ujisalimishe. Ni ishara nzuri kwamba unapaswa ujisalimishe mwenyewe.

Sasa yote ufanyayo, kaka au dada (anaweza akawa mtu mdogo au mzee, vyovyote iwavyo) ulisema…..Hawawezi wakajua wenyewe hivyo waweze kujisalimisha kikamilifu. Jiachilie kabisa wewe mwenyewe. Bwana mawazo yangu na vyote mimi nilivyonavyo napenda nivikupe wewe, maisha yangu, nakupa wewe kwa ajili ya kazi yako. Nichukue, Bwana, na unitumie kama nilivyo” Na ni rahisi hivyo.

Angalia hapa, hapa yupo msichana mdogo anayejinyonganyonga mwenyewe chini kule barabarani. Hapa pana kijana mdogo macho yake yananasa hilo yeye ni mwanachama wa kanisa; yeye ni mpentecoste au chochote kile alicho; lakini kitu cha kwanza unajua hakuna ile nguzo pale yakushikilia.

Msichana atasema ”Aloo” mvulana huyo ana nywele zilizolala na anaonekana ni wa kuvutia mabega yaliyonyooka ya mvulana mwanaume, pengine amefundishwa kuishi kwa usahihi msichana huyo anatembea kuelekea kwake. Anaweza akawa ni mhubiri….Jambo la kwanza unajua…..ni nini? Huu wa nje hapa, tamaa za mwili, na roho chini pale, ikiwa imepakwa mafuta, inasema “usifanye hilo, usifanye hilo” lakini itafanya nini? Itaenda ikizunguka, pale pakushikilia; huyo anakwenda jambo la kwanza unajua anajaribu kuweka tarehe na yule msichana yeye anahatia ya kufanya uzinzi ikiwa atamgusa huyo msichana au la. Lakini mwana wa Mungu aliyezaliwa mara ya pili kweli ……Amen.

Huwezi kulifanya hilo mwenyewe ni haiwezekani kabisa kwa mwanaume mwenye damu-nyekundu atembee mbele ya mwanamke kama hivyo pasipo jambo fulani kutokea. Lakini kama kuna kitu fulani kule ndani, kile kitu fulani kidogo cha kuzaliwa mara ya pili pale…..Ingawa mtu huyo amepiga makelele, amenena kwa lugha, ameruka na kucheza, na kila kitu, amepakwa mafuta na roho amefanya ishara zote na maajabu Mungu alisema ndani pale, ni kwa roho Yangu……..

Yesu alisema. “Wengi watakuja kwangu katika siku ile na kusema Bwana sikutoa unabii kwa jina lako? Sikutoa pepo kwa jina lako? Sikutoa……”Alisema, sikuwajua ninyi kamwe ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu” (Matayo 7:21-23) uovu ni nini? Jambo fulani unalojua kulitenda na hulitendi “Sikuwajua ninyi kamwe, ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu”.

Lakini kilindini ndani ya mtu huyu kama ile nguzo ndogo yakushikilia ingekuwa pale ile mbegu ya Mungu iliyochaguliwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, sijalishi hunatokea nini; itamshikilia; iko pale kukaa (kudumu).

Neno la Mungu kamwe haliwezi kushindwa litashinda bila kujali ni kitu gani. Ndipo nilijua kwamba kuna kitu fulani ndani ya mawazo yote. Kitu fulani ndani ya misisimko yote vitu vyote kama hivyo; kulikuwa na mtu wa ndani aliyeshikilia pale katika saa ile (2 kor 4:16) hakuna chochote kingine kingefanya hilo. Kila wazo, kila kitu kiwezacho kuonekana kila kitu kingethibitisha hilo kwamba siyo sahihi, na kwamba nilikuwa makosani, lakini Neno la Mungu lililokuwa limekusudiwa kabla ya kuwekwa misingi ya dunia lilishikilia ndani.

Kaka, dada ngoja nikuambie hicho ndicho kitu pekee. Usijaribu kuwazia hilo upate jibu. Usijaribu kuweka nywele ndefu kwa sababu nimesema hivyo. Usijaribu kufanya mambo hayo kwa sababu tu, katika mwili wako….usijaribu kufanya hivyo ili kujaribu kukubaliana lakini subiri tu mbele za Bwana mpaka kitu fulani kilindini kule ndani……

Wengi wenu wanafikiri kwa sababu una nywele ndefu, hiyo inamaanisha utakwenda mbinguni hiyo haimaanishi hivyo. Wengi wao hufikiri, kwa sababu ni mwanamke aliye na maadili mema, utaenda….haimaanishi hilo. Wengi wao hufikiri kuwa kwasababu makanisa yao na wako katika hili na wako katika makundi haya makubwa na madaktari wakubwa wa theolojia. Hiyo haimaanishi hilo unaona? Wengi wanafikiri kwa sababu wamenena kwa lugha, wanaye Roho Mtakatifu hiyo haimaanishi hilo, ingawa Roho Mtakatifu ananena kwa lugha, Lakini mpaka kitu kile cha kweli Roho Mtakatifu halisi aliye pale akubaliane na kila Neno…….

Kama Roho Mtakatifu aliyendani yako anakufanya unene kwa lugha, angalia nyuma pale na hakubaliani na Neno lote, hapo sasa ni roho isiyo sahihi unaona? Inabidi ije kutoka ndani, ambayo ni Neno Tangu mwanzo katika mwanzo wa uumbaji wa Mungu wakati Mungu alipoanza kuumba na kukuleta wewe katika maisha…..unaona, ulianza nyuma pale kama mbegu na ukaendelea chini mpaka ulipo sasa na hapo sasa wote mlikuwa ndani ya kristo halafu kristo alipokufa, alikufa kuwaokoa ninyi wote (Rum 6:6; 2 kor 5:14) na wewe u sehemu ya dunia hii. Na itawezekanaje Biblia….yote hiyo kanuni juu ya kanuni mstari juu ya mstari, hapa kidogo na hapa kidogo, hakuna hata yodi moja au kidogo itakayoshindwa….itakuwaje katika dunia wewe, ukiwa sehemu ya Neno usikubaliane na lote au sehemu yake?

Ndugu Brahamu je shetani aweza kutumia karama ya kunena kwa lugha au unabii katika mtu aliye na Roho Mtakatifu? Hilo ni moja ya mazuri si ndiyo? Ndiyo, Bwana. Inabidi iangaliwe kwa karibu sana. Katika 1korintho 14:26-29 tunaona kwamba karama yoyote katika kanisa inabidi kwanza ijaribiwe unaona? Inabidi uangalie kwa sababu roho ovu hupenya ndani kwa sababu kumbuka mvua hunyesha kwa wenye haki na wasio haki (matayo 5:44-45) mvua ile ile iliyotumwa kuivisha ngano inaivisha magugu. Maji yale yale wangapi wanajua hilo? Sasa, hilo linapaswa kuweka wazi uzao wa nyoka hapo. mtoto huyu alivyokuja. Ninajaribu kuliokota hapa kulipata kabla ya muda wangu haujaisha lakini siwezi kuliona kwa hiyo ni kwa namna gani huyo mtoto alikuwa uzao wa nyoka? Unaona.

Mungu anazo kanuni au sheria, sasa, katika hili katika sheria za roho ya uzima inabidi uangalie kwa sababu shetani anapenyeza ndani.

Na Paulo wakati mtu fulani amefunuliwa jambo, ilibidi pawe na watu wawili au watatu kulipima kabla kanisa halijaambiwa.

Nataka niulize….hakuna anayepaswa kusema hiki kuna watu kwa uchache kumi na tano au ishirini wako wameketi hapa wana hatia ya kufikiria kwamba mimi ni yesu Kristo wanawezaje kufanya hivyo? Nilikuwa pamoja nao mpaka nilipotambua kwamba Mungu aliniambia mimi kuwa ni roho. Na watu hawa nilisema…..Na watu hawa waliniamini mimi, kwa kila Neno nilisema, “mtaniaminije mimi kama

nikiwaambia? “ Ndipo tukaenda kwenye Neno; ndipo walianza kuona wakasema “Vema ni kweli hatukuamini wewe, au tungesikiliza kile ulichotuambia” unaona hilo?

Lakini walifikiri kuwa wako sahihi waaminifu unaona? Na moja ya roho hizo inakuja kwako, ambaye unaye, utaamini kwa hakika sijali, hakuna anayeweza kukuambia tofauti unaona? Haijalishi Neno linasemaje juu ya hilo, vema, hutaamini tu kwa vyovyote vile; utaendelea kama unataka kuwa hivyo, endelea na nitakuwa na njia yangu” unaona, hiyo inaonyesha umepakwa mafuta na roho isiyo sahihi.

Roho wa Mungu ata…..vema unasema “unasemaje juu yako wewe, ndugu Branham? Niko tayari kwa mtu yeyote anionyeshe mimi kilicho sahihi na kisicho sahihi, lakini inabidi iwe ni Neno haiwezekani kusema….lazima kitoke kwenye Neno hapa sasa ndipo mihuri ilipofunguka. Na kamwe msije mkawa na shaka kama ni muhuri utajionyesha wenyewe kutoka mwanzo mpaka ufunuo. Kwa hiyo mihuri hiyo. Hamumpendi yeye?

Watu wengi wanyoofu wanaenda wanajiunga na dhehebu au kundi au kikundi cha aina fulani na pale wanakufa kiroho Huwezi ukawaambia chochote. Hayo mambo yasiyo, yanaingizwa ndani yao “ kwa nini askofu huyu alisema hivi na huyu alisema hivi” waonyeshe wao hapa katika Neno la Mungu ambalo ni HII ASEMA BWANA “lakini mchungaji wetu……” sijali mchungaji wenu amesemaje usijali ninasemaje au mtu mwingine anasemaje kama iko kinyume na Neno la Mungu lililothibitishwa la saa na wakati, ujumbe na kadhalika sahau hilo kaa mbali nalo na nitapaswa kusimama mbele ya kila mmoja wenu katika siku ya hukumu na mnajua hilo na singesema jambo kama hilo hata kidogo kwa kujua ni mtu mzima sasa ili…..siyo kwamba ninajua kitu fulani lakini yeye anajua ninafuata tu kile anachosema (Matayo 24:24-25).

**Nukuu za Kiingereza**

“Maswali na majibu “(64-0823M), Q-No.278, cod uk. 982 Nawe hujui, uk 23,28 / Maswali na majibu 64-0823E, Q-No 292, COD uk 1022/ “Ufunuo sura ya tano sehemu ya 2”, Aya 232
“ Maswali sura ya tano sehemu ya 2”.Aya 232
“Kujaribu kumfanyia Mungu kazi” (65-0718M) Aya 137

Jiwe la kiroho la kujengea na. 118 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.
(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*
*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*